



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MADINI

## Matumizi Salama ya Baruti



## **UTANGULIZI**

Baruti ni kemikali iliyo na uwezo wa kulipuka na kulipua vitu mbali mbali ikiwemo miamba. Tahadhari isipochukuliwa kuhusu matumizi sahihi ya baruti madhara makubwa yanaweza kutokea. Madhara hayo ni pamoja na ajali mbali mbali zikiwemo uharibifu wa mali, ulemavu au watu kupoteza maisha

## **MATUMIZI SALAMA YA BARUTI**

Matumizi salama ni yale yanayozingatia afya bora za watu, usalama wa watu, utunzaji wa mazingira, usimamizi bora wa vifaa vya kazi, mali na miundombinu ya migodi.

Matumizi ya baruti husimamiwa na Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na kuongozwa na Kanuni za Mwaka 1964,

## **TARATIBU ZA KUPATA NA KUMILIKI BARUTI KISHERIA.**

Kuingiza baruti kutoka nje ya nchi (import of explosives).

Ili kuingiza baruti kutoka nje ya nchi mtu anahitajika awe na;

- Kibali cha Kuingiza Baruti nchini (Import Permit) kutoka Wizara ya Madini
- Sehemu ya kuhifadhia baruti (Magazine,
- Mtaalamu wa baruti mwenye cheti cha ulipuaji (Blasting Certificate)

## **Kununua au kupata baruti hapa nchini.**

Ili kununua baruti kutoka kwa makampuni yaliyoidhinishwa kuagiza au kutengeneza na kufanya biashara ya baruti hapa nchini unatakiwa uwe na ;

- Sehemu ya kuhifadhia baruti
- Leseni ya Kununulia au Kumiliki Baruti kutoka Wizara ya Madini.
- Mtaalamu wa baruti mwenye cheti cha kulipulia (Blasting Certificate)

## **Kutengeneza baruti hapa nchini.**

Kwa makampuni yanayotaka kutengeneza baruti zao, ili watengeneze baruti zao wanahitaji kupewa Leseni ya Kutengeneza Baruti (Licence to Manufacture Explosives) kutoka Wizara ya Madini. Utengenezaji wa baruti huongozwa na Kanuni za Baruti (Utengenezaji) za Mwaka 2019.

## TARATIBU ZA KUHFADHI BARUTI.

Kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha Sheria ya Baruti ya mwaka 1963 kuna aina tatu za maghala ya kuhifadhi baruti ambazo ni bohari ( Magazine), Stoo na Sanduku.

Ili kuagiza baruti kutoka nje ya nchi mtu anahitajika awe na



### **Bohari (Explosive magazine)**

Bohari ya baruti huhifadhi baruti (Fracture explosive) yenye uzito unaozidi Kg 450 au fataki (detonators) inayazidi vipande laki nne (400,000).

Kabla ya kujenga bohari la baruti, muhusika anatakiwa kuomba kibali cha kujenga bohari hiyo kutoka kwa Kamishina wa Madini kulingana na kifungu cha 31 cha Sheria ya Baruti.

Leseni ya bohari la baruti hutolewa na Kamishina wa Madini baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi inayoridhisha kutoka kwa Mkaguzi wa Baruti na baada ya kulipiwa malipo ya leseni hiyo.

### **Ghala aina ya Stoo( Explosive store)**

Stoo ya baruti huhifadhi baruti zenye uzito hadi Kg 450 au lwapo ghala hii itahifadhi fataki, basi idadi ya fataki ambazo zinaruhusiwa kuhifadhiwa humo zisizidi 400,000.

### **Ghala aina ya Sanduku( Explosive storage box)**

Sanduku la baruti linaruhusiwa kuhifadhi baruti zenye uzito usiozidi kilo 45 au lwapo ni fataki kiasi kisichozidi 10,000.

Sanduku la baruti hutengenezwa kulingana na maelezo ambayo hutolewa na Mkaguzi wa Baruti na kukubaliwa na Kamishina wa Madini.

Kabla ya kutoa leseni, Mkaguzi anaweza kuamua kufanya ukaguzi

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTUNZAJI WA BARUTI

- Baruti huweza kuharibika iwapo itakaa kwa muda mrefu bila kutumika katika hali ya hewa ya joto au unyevunyevu
- Athari za kuharibika ni pamoja na kupoteza uimara wake na kuwa rahisi kulipuka baada ya kushikwa au kusukumwa kidogo; kupoteza nguvu zake za kupasua miamba
- Watumiaji wanashauriwa kuwa waangalifu kuangalia expiring dates za baruti na kuhakikisha baruti zinatumiwa kabla ya tarehe hiyo.
- Hairuhusiwi kuhifadhi fataki na baruti kwa pamoja kwakuwa fataki ni viwashio ambavyo huwasha baruti nyingine.
- Usivute sigara au kuruhusu viberiti au moto wowote unaowaka ndani au karibu na ghala la baruti au wakati unaposhughulikia baruti na fataki.
- Hairuhusiwi kuhifadhi baruti katika makazi ya watu au sehemu tunazofanyia kazi. Umbali wa sehemu ya kuhifadhi baruti kutoka kwenye makazi ya watu au sehemu tunazofanyia kazi uendane na vipimo vilivyowekwa kwenye jedwali Na.3 kwenye kanuni ya baruti ya mwaka 1964.

AINA YA LESENI/KIBALI	USD	TSH
Maombi ya cheti cha kulipua		200,000
Ada ya leseni ya kutengeneza baruti mgodini Na maeneo mengine	1000 200	
Kuhuisha cheti cha kulipua baruti		200,000
Ada ya majaribio ya cheti cha kulipua baruti		50,000
Maombi ya kibali cha kuingiza baruti au kusafirisha nje ya nchi.	500	
Maombi ya kibali cha kuuza baruti	500	
Ada ya kibali cha kuuza baruti	200	
Leseni ya kununua baruti (Licence to purchase or acquire explosives) kwa kiasi kisichozidi tani 1.		100,000
Leseni ya kununua baruti(Licence to purchase or acquire explosive) kwa kiasi kinachozidi tani 1.		200,000
Kibali cha kupitisha baruti	500	
Ada ya maombi leseni ya Bohari ya kuhifadhi baruti		500,000
Ada ya mwaka ya leseni ya Bohari ya kuhifadhi baruti		500,000